

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA**

SHULE YA SEKONDARI BOSHA
S.L.P 16
MARAMBA

KUMB NA BSS/S...../JI/2020

KWA:.....

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BOSHA 2021

1.0.Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kuijunga na shule hii kidato cha kwanza mwaka 2021. Hongera sana ni matumaini yangu kuwa UTAUENZI uchaguzi huu kwa kufanya kazi ya kiuwanafunzi (kusoma) kwa bidii na kwa nidhamu. Shule itafunguliwa siku ya jumatatu tarehe.....masomo yataanza tarehe.....kwa kidato cha kwanza hivyo basi kila mzazi amlete mwanaae.

2.0.SARE ZA SHULE

- 2.1.Mashati 2 meupe/vazi la hijabu liwe jeupe lisiloangaza
- 2.2.Viatu vyeusi vya kamba, visigino vifupi
- 2.3.Soksi nyeupe
- 2.4.Suruali/sketi 2 mzazi atajinunulia mwenyewe baada ya kupewa aina ya kitambaa na mshono siku ya kuchukua barua hii
- 2.5.Sketi ya marinda yenyre rangi damu ya mzee
- 2.6.Suruali ni ya rangi ya damu ya mzee

3.0.MAHITAJI

- i. Madaftari 10 makubwa na madogo 3
- ii. Mkebe wa hisabati
- iii. Begi la kubebea madaftari
- iv. Jembe na panga kwa wavulana reki, ndoo na fagio kwa wasichana

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI BOSHA

.....
**CYPRIAN A. TABANI
MKUU WA SHULE**

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BOSHA

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI

- i. Mimininakubali/sikubali kujiunga na shule ya sekondari Bosha katika kidato chanitafika shule bila kuchelewa. Ninakiri kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- ii. Anuani yangu ya kudumu ni
.....
.....
- iii. Saini ya mwanafunzi.....tarehe.....

B: SEHEMU YA MZAZI

- i. Mimi.....nimekubali/sijakubali mtoto wanguajiunge na shule ya sekondari Bosha ninaahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shulenii kama ulivyoagiza pamoja na kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada. Michango yote na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- ii. Anuani yangu ya
kudumu.....
.....
.....
- iii. Saini ya Mzazi/Mzazi.....tarehe.....

(TAFADHALI NJOO NA FOMU HII UTAKAPOKUJA SHULENI IKIWA IMEJEZAWA).

4.0.Sheria na kanunni muhimu za shule hii ni;

- 4.1.Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na-25 ya mwaka 1987. Aidha inazingatia miogozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingaitia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripia shulenii.
- a. Heshima kwa viongozi wazazi na wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
 - b. Mahudhurio katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
 - c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
 - d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
 - e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wakao katika shule hii
 - f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
 - g. Kuвая sare ya shule wakati wote unaotakiwa
 - h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- 4.2.Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule ni;
1. Wizi
 2. Uasheratia na ushoga
 3. Ubakaji
 4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
 5. Kupigana au kupiga
 6. Kuharibu kwa makusudi mali umma
 7. Kudharau Bendera ya Taifa
 8. Kuoa au kuolewa
 9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
 10. Kutoa mimba
 11. Kugoma, kuchochea na kuongeza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
 12. Kukataa adhabu kwa makusudi
 13. Mwanafunzi kuwa na simu mkononi